Imani na kufanya Ukristo kufanya kazi.

TAFADHALI BIBLIA YAKO IWE IMEFUNGULIWA NA UJARIBU KUANGALIA VIFUNGU VYOTE REJEA.

Mpaka sasa katika masomo yetu mara nyingi sana tumekuwa tukitumia neno "IMANI. Ni wakati muafaka sasa kuangalia na kutafakari nini waandishi wa Biblia walikusudia kutuelewesha juu ya neno hili. Linaweza kutumiwa katika lugha ya kawaida kwa njia mbalimbali. Utaratibu wa kuabudu unaweza kuitwa "Imani; Iwapo tungetembea katika njia nyembamba na kuvuka korongo au mto mdogo, tungehitaji imani ambayo ni madhubuti kuweza kuubeba uzito wetu.

Paulo katika Waraka wake kwa Waebrania sura ya 11 mstari wa 1 anatupatia maelezo ya "imani". Maneno haya yanachukuliwa kutoka katika Biblia ya toleo mpya la Kimataifa The New International Version ya Biblia. "Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo ni bayana ya mambo yasiyoonekana, Maana kwa hayo watu walishuhudiwa". Sasa unaelewa kutokana na masomo uliyomaliza kwamba katika Agano la Kale Mungu alionekana kuwa karibu sana na Abrahamu na familia yake mpaka kufikia wakati wa Manabii. Watu walioishi siku zile hawakuwa mbali sana na nyakati za mojawapo ya maajabu. Labda ilikuwa rahisi kwao kuwa na imani kwa Mungu na ahadi zake. Mungu alitarajia watu hao kuwa na "imani" na kuwazawadia walipoitikia.

Nyakati za Yesu miujiza yake ndiyo iliyowashawishi watu wa nchi ya Israeli kuwa alikuwa mwana wa Mungu ambaye ni Mesihi. Angalia Injili ya Yohana sura ya 11 mistari ya 44 na 45 kuwa mfano wa haya.

Leo hatuna maajabu ya waziwazi kama kuachana kwa Bahari Nyekundu hata kuhusu Waisraeli kuyatoroka majeshi ya Misri; Angalia kutoka sura ya 14 hususani mstari wa 13. Hatuna Manabii wa Mungu wanaotembea katika nchi na hatuwezi kusimama na kuangalia miujiza kama ile iliyofanywa na Yesu. Wewe ulichonacho ni Biblia, aghalabu matukio yote, ahadi na maonyo yaliyoandikwa humo kwa nguvu za Mungu ili tuweze kusoma. Kwa kielelezo cha kudumu cha kukukumbusha mpango wa Mungu kwa dunia hii na ahadi yake kwako binafsi kuwa mshiriki wa wakati ujao. Kwa hiyo leo imani ni uthibitisho wa ndani unaokuwanao katika mawazo yako.

Utakuwepo huo kwa sababu ya yale unayoyasoma katika Biblia yako na kwa sababu ya mambo yale ulivyojifunza kutoka kwa wengine amba pia wana imani katika Neno la Mungu.

Ninachotaka sasa kufanya ni kukuonyesha kwamba Mungu pia anatutarajia tuiweke imani katika vitendo. Mtume Yakobo katika Waraka wake anatueleza haya. Tazama sura ya 2 mistari ya 14 hadi 18. Je unakubali kuwa uhusiano kati ya imani na vitendo ni wazi? Jambo lingine muhimu la kutafakari linapatikana katika Sala ambalo pia ni unabii, limo katika kitabu cha kwanza cha Samueli sura ya 2 mstari wa 3. Humo tunasoma kuwa Mungu anatuangalia na kufikiria juu ya matendo yetu yote. Kwa hiyo yale tutendayo kwa sababu ya kuwa na imani ni muhimu sana.

Mungu anajua kwamba tunahitaji msaada ili kuyatenda haya na tumepewa mifano mingi jinsi imani inavyoweza kuwa katika vitendo. Kuna mifano miwili katika kifungu tunachosoma katika Waraka wa Yakobo ilikuwa katika sura ya 2 na sasa tuangalie mistari ya 21 hadi 24.

Kama ukifungua kitabu cha Mwanzo 22 na kusoma mistari 1 hadi 18 humo unaweza kusoma matukio yote. Kuainisha kwa ukamilifu imani ya Ibrahimu huna budi kukumbuka kwamba Mungu alikuwa ametoa ahadi maalumu kwake alipotokeza katika nchi ya Ur. Tunaweza kusoma haya katika kitabu cha Mwanzo sura ya 12 mistari ya 1 hadi 3. Ahadi hii ilimtaka Ibrahimu kuwa na mtoto ili familia yake iweze kuwa Taifa kubwa. Hatimaye alipata mtoto, Isaka yeye na mkewe wakiwa wazee sana. Haya yanatusaidia sisi kuelewa jinsi imani ya Ibrahimu ilivyojaribiwa alipoambiwa kumtoa kafara Isaka. Paulo katika Waebrania sura ya 11 mistari ya 17 hadi 19 anatuambia Ibrahimu alikuwa na mawazo gani alipokuwa akielekea mlimani. Isaka alikuwa muhimu katika ahadi aliyoweka Mungu, bila yeye ahadi isingelitimizwa kama ilivyokuwa yeye afe; Mungu angemrejesha katika uhai. Wewe ukijifanya kuwa katika nafasi ya Ibrahimu, utabaini jinsi gani imani yake ilivyokuwa na nguvu.

Jambo lingine muhimu katika tukio hili ni kwamba Mungu alifanya haya sio tu kumjaribu Abrahamu, bali Mungu alikuwa tayari anajua ushupavu wa imani yake na unaweza kuona hili katika kitabu cha Mwanzo sura ya 15 mistari ya 3 hadi 6. Amri ya kumtoa dhabihu Isaka ilikuwa kumfundisha Abrahamu jinsi Mungu alivyokusudia kumkomboa mwanadamu. Ilimfundisha Abrahamu kwamba siku

moja katika nyakati zijazo Mungu kama Baba atamruhusu mwanae pekee kuwa shabaha kwa ajili ya dhambi za Ulimwengu. Kwamba angefanya uwezekano wa misamaha, ufufuko na uzima wa milele kwa wanaume na wanawake wenye imani katika Mungu na mwanae Yesu Kristo.

Mfano mwingine uliotolewa na Yakobo ni ule wa Rahabu. Kwa mara ya kwanza bila ya matarajio mtu wa Mataifa ambaye wala hakuwa Myahudi kahaba aliyekuwa anaishi katika Jiji la Kanani huko Jeriko. Alikuwa ni mtu pekee aliyeamini katika Mungu wa Wayahudi. Hata hivyo, Rahabu alikuwa anaelewa kuwa watu wengi waliokuwa wamejenga makambi yao katika ufuko wa mto Jordani, walikuwa warejeshewa nchi yao ya kale, nchi ambayo Abrahamu alipewa na Mungu. Wewe mwenyewe unaweza kusoma ili upate kujua kitu gani kilitokea katika kitabu cha Joshua sura ya 2. Jinsi maajabu ya kuta za jiji zilivyoanguka na Rahabu na familia yake peke yake walivyookolewa kwa sababu ya kuhatarisha maisha yake ili kuwaokoa majasusi ya Kiisraeli. Tukio hili bila shaka halikuwa la kawaida na ndiyo maana Yakobo na Paulo walitumia kama mfano wa imani.

Katika Waebrania sura ya 11 kuna mifano mingi ya imani katika vitendo na sasa nataka kuangalia mwingine mmoja zaidi. Noah aliishi katika nyakati zilizokuwa na machafuko mengi miongoni mwa watu wa ustaarabu wa Kale. Angalia mwenyewe kitabu cha Mwanzo vifungu vya 6, 7 na 8. Angalia hususani sura ya 6 mistari ya 5 hadi hadi 7, ona ni miaka mingapi ilimchukuwa Nuhu kujenga Safina hii kubwa; sura ya 5 mstari wa 32 na sura ya 7 mstari wa 6. Miaka mia moja ni muda mwingi sana kwetu sisi lakini kwa Nuhu aliyeishi miaka 950 haikuwa hivyo. Bilashaka hakuna mtu mwingine aliyewahi kuunda mtumbwi mkubwa kama huu kabla. Katika miaka yote hii, Nuhu alimbidi kate miti mikubwa, ajifunze namna ya kutengeneza misumeno, kukata na kuziweka katika umbo mbao ambazo aghalabu wakati wa utengenezaji atazisawazisha na kuziunganisha vizuri ili zisivuje maji. Mti huu wa mvinje ilikuwa lazima uwe mkubwa sana na uwe mahali pa usalama kwa watu na wanyama, ndege na wadudu kwaa muda mrefu wa mwaka mmoja.

Katika kutumia nguvu nyingi wakati wa miaka ile ya kuunda Safina, Nuhu aliongozwa na imani katika Mungu. Paulo anajumuisha katika mfano huu wa muhimu sana kwetu sisi katika Waebrania Sura ya11 mstari wa 7.

Mpaka sasa tumejifunza nini katika somo hili?
- Kwamba imani ni kuamini kuwa Mungu yuko na kwamba wakati
wowote atafanya kile alichoahidi.
- Kwamba haitoshi kusema tu tunaamini, Mungu daima anajua kuwa ni kweli.
- Kwamba imani peke yake haitoshi, inatubidi kuiweka katika vitendo katika maisha yetu.
- Kwamba Mungu wakati mwingine anatutarajia sisi kuendelea kaatika kitendo hicho kwa miaka mingi.

Kama unafikiria kuamua kamainkubidi ubatizwe au kama tayari umemkubali Yesu katika ubatizo, utatakiwa kuelewa ina maanisha ni siku hadi siku. Je umeiwekaje imani yako katika vitendo? Hapa kuna mapendekezo kutoka kwa Paulo katika waraka wake kwa Warumi sura ya 12 mistari ya 9 hadi 18. Soma kwa uangalifu na tafakari iwapo yanaweza kukuhusu katika maisha yako. Paulo anatuambia kuwa tuheshimu Serikali za nchi yetu hata kama imejaa rushwa. Hii ina maana ya kuwa tuheshimu nguvu za sheria na utengamano. Angalia sura ya 13 mistari ya 1 hadi 5. Hii pi inajumuisha ulipaji wa kodi kwa uaminifu, mistari ya 6 na 7.

Maagizo yaliyo mengi na yenye nguvu yanatoka kwa Yesu katika Mathayo sura ya 25. Soma mistari ya 31 hadi 40. Hapa Yesu anatueleza jinsi tunavyopaswa kuyaweka mafundisho yake yafanye kazi katika maisha yetu. Ni muhimu kuyakumbuka maneno haya.

Yesu anazungumzia juu ya siku ya hukumu kwa kuwa katika siku ile hatutajaribu kiasi gani tunaelewa, lakini kiasi gni tumejaribu kuyafanya mafundisho yake katika matendo.

CBM Publishing, 32 Blenheim Rd, Far Cotton, Northampton NN4 8NW United Kingdom
PO Box 2950, Mbeya, Tanzania (East Africa)